> *Isaya 46:3 “Nisikilizeni, enyi wa nyumba ya Yakobo, ninyi mlio mabaki ya nyumba ya Israeli, mliochukuliwa nami tangu tumboni, mlioinuliwa tangu mimbani;*
>
> *4 na hata uzee wenu mimi ndiye, na hata wakati wenu wa mvi nitawachukueni; nimefanya, nami nitachukua; naam, nitachukua na kuokoa”.*

Mstari huu wa faraja unatuonyesha fadhili za Mungu jinsi zilivyo nyingi kwa watu wake, Anaonyesha jinsi asivyoweza kuwaacha watu wake, tangu wakiwa tumboni mwa mama zao hadi kufikia uzee wao. Kila hatua ya maisha yupo nao, kila pito liwe rahisi au liwe gumu yupo nao, wakiwa watoto, wakafikia ujana, kisha nguvu zikaisha wakiwa wazee, Mungu yupo nao. Haleluya.

Daudi alilitambua hilo pindi alipoishiwa nguvu zake, akaandika…

> *Zaburi 37:25 “Nalikuwa kijana nami sasa ni mzee, Lakini sijamwona mwenye haki ameachwa Wala mzao wake akiomba chakula”.*

Hivyo huna haja ya kuhofu kesho yako itakuwaje au uzee wako utaishaje, maadamu upo na Bwana, maadamu unamtumikia, siku hizo zikifika, atakuhifadhi Mungu wako. Mwingine anasema mpaka sasa sina mfuko wa mafao, na nguvu zangu zinakaribia kuisha, ni nani atakayenisaidia, ni nani atakayekuwa karibu na mimi? Jibu ni kuwa  Bwana ndiye atakayekuwa karibu na wewe. Kwasababu tangu zamani ulimtumainia. Lakini hata kama utakuwa na mali, huwezi kuwa na raha moyoni wakati huo endapo Kristo hayupo nafsini mwako sasa.

Hivyo wekeza maisha yako kwa Bwana sasa, ili kesho yako pia iwe na matumaini na raha tele. Ikiwa wewe ni kijana wakati huu uliopo, mtafute muumba wako, upokee WOKOVU kwa kumaanisha kabisa kuuacha ulimwengu, mtumikie Mungu, kimbia kweli kweli tamaa za ujanani, kabla zile nyakati mbaya za hatari hazijafika, Kwasababu maandiko yanasema kuna siku-mbaya mbeleni zitawakumba watu ambao hawakumcha Mungu tangu zamani.

Mhubiri 12:1 “Mkumbuke Muumba wako siku za ujana wako, Kabla hazijaja siku zilizo mbaya, Wala haijakaribia miaka utakaposema, Mimi sina furaha katika hiyo”.

Ikiwa upo tayari kutubu dhambi zako leo , na kumkaribisha Bwana Yesu maishani mwako, basi bofya hapa kwa mwongozo wa sala hiyo ya toba >>>> KUONGOZWA SALA YA TOBA[1]

Bwana akubariki.

Tafadhali shea na wengine ujumbe huu;

Pia Kwa maombezi/ Ushauri/ Maswali/ Whatsapp:
Tuandikie katika BOXI la Maoni hapo chini au
Piga namba hizi: +255693036618 au +255789001312

Mada Nyinginezo:

TUTAMKARIBIA MUNGU KWA IDADI YA MVI ZETU ROHONI.[2]

Je! Wana wenu huwatoa kwa nani? maana yake ni nini?[3]

NINYI AKINA BABA MSIWACHOKOZE WATOTO WENU[4]

UFANYE WEMA WAKO KATIKA MAARIFA.[5]

ANGALIENI MWITO WENU.[6]

Praitorio ni nini? Na Kwanini ilikuwa ni najisi kwa wayahudi kuingia humo? (Yohana 18:28)[7]

Afadhali mtu akutwe na dubu aliyenyang’anywa watoto wake.[8]

Rudi nyumbani[9]

Share on:
WhatsApp

Endnotes:

1. KUONGOZWA SALA YA TOBA: https://wingulamashahidi.org/2020/07/22/kuongozwa-sala-ya-toba/
2. TUTAMKARIBIA MUNGU KWA IDADI YA MVI ZETU ROHONI.: https://wingulamashahidi.org/2021/02/22/tutamkaribia-mungu-kwa-idadi-ya-mvi-zetu-rohoni/
3. Je! Wana wenu huwatoa kwa nani? maana yake ni nini?: https://wingulamashahidi.org/2020/10/28/je-wana-wenu-huwatoa-kwa-nani-maana-yake-ni-nini/
4. NINYI AKINA BABA MSIWACHOKOZE WATOTO WENU: https://wingulamashahidi.org/2023/04/06/ninyi-akina-baba-msiwachokoze-watoto-wenu/
5. UFANYE WEMA WAKO KATIKA MAARIFA.: https://wingulamashahidi.org/2023/01/17/ufanye-wema-wako-katika-maarifa/
6. ANGALIENI MWITO WENU.: https://wingulamashahidi.org/2021/01/08/angalieni-mwito-wenu/
7. Praitorio ni nini? Na Kwanini ilikuwa ni najisi kwa wayahudi kuingia humo? (Yohana 18:28):

https://wingulamashahidi.org/2023/07/18/praitorio-ni-nini-na-kwanini-ilikuwa-ni-najisi-kwa-wayahudi-kuingia-humo-yohana-1828/

8. Afadhali mtu akutwe na dubu aliyenyang’anywa watoto wake.: https://wingulamashahidi.org/2022/10/16/afadhali-mtu-akutwe-na-dubu-aliyenyanganywa-watoto-wake/
9. Rudi nyumbani: https://wingulamashahidi.org